Maswali

1. Abramu aliishi wapi?
2. Watu wa huko waliabudu nini?
3. Mungu aliambia Abramu afanye nini?
4. Mungu aliahidi Abramu nini?
5. Nani alienda na Abramu?
6. Mungu aliwapeleka mpaka nchi gani?
7. Abramu alifanya nini alipofika kwa nchi ya Kanaani?
8. Mungu alitimiza ahadi zake kwa Abramu namna ngani?
9. Abramu ataishi lini milele kwa nchi yenye Mungu alimwahidi?
10. Mungu anatuahidi sisi nini?

Majibu

1. Abramu aliishi kwa nchi ya Uru.
2. Watu wa Uru waliabudu mungu mwezi. Hawakuabudu Mungu wa kweli.
3. Mungu aliambia Abramu aiache nyumba na familia yake Uru na aende kwa nchi yenye Mungu atamwonyesha.
4. Mungu aliahidi Abramu kwamba wazao wake watakuwa taifa kubwa, atakuwa na sifa na watu wote ulimwenguni watafurahia mmoja wa wazao wa Abramu.
5. Abramu alienda na mkewe Sarai na mpwa wake Lutu.
6. Mungu aliwapeleka mpaka nchi ya Kanaani (inaitwa Israeli sasa).
7. Abramu alijenga madhabahu na akatolea Mungu sadaka ya mwana kondoo.
8. Wazao wa Abramu ndiyo taifa la Wayahudi, Abramu ana sifa, Yesu ni uzao wa Abramu, atakapokuja kusimamisha Ufalme wa Mungu hapa duniani, kila mtu atafurahi.
9. Abramu ataishi duniani milele wakati Yesu atarudi.
10. Hata sisi tutaishi kwa Ufalme wa Mungu hapa duniani ikiwa tutampenda.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3

3 Mungu anamwita Abramu

Marejeo

Mwanzo 12:1 – 6



URU

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Abramu alikuwa na imani kuu kwa ahadi za Mungu. Alitii na kutoka nyumbani kwao na kwenda penye Mungu alitaka.

Maneno maalum

3.1 Abramu + Uru + mungu mwezi + Abramu alipenda Mungu + ondoka Uru + enda nchi ngine
3.2 Ahadi za Mungu + taifa kubwa + ana sifa + wote wafurahi
3.3 Abramu alienda + Sarai + Lutu + safari ndefu + Kanaani
3.4 Madhabahu + shukuru Mungu + ahadi nyingine + nchi milele
3.5 Mungu alitimiza ahadi + Yesu atarudi + Ufalme wa Mungu duniani + kila mtu na furaha ingine

3.1 Abramu aliishi kwa mji mkubwa uliokuwa na michengo na bustani nzuri. Huo mji uliitwa Uru. Abramu aliishi kwa nyumba nzuri na alikuwa tajiri. Watu walioishi Uru hawakupenda Mungu. Waliabudu mwezi badala ya Mungu. Kulikuwa na Hekalu kubwa ya mungu mwezi huko Uru. Lakini Abramu hakuamini kwa mungu mwezi. Alipenda Mungu wa kweli na alijaribu kumfurahisha.

Siku moja Mungu aliambia Abramu, "Wacha nyumba yako na familia yako hapa Uru. Wacha mji wako na marafiki zako na usafiri kwa nchi nyingine. Nitakuonyesha njia."

Mungu alitaka kuondoa Abramu kutoka Uru kwa watu walioabudu mwezi na waliofanya mambo maovu. Tena Mungu alitaka kumjaribu Abramu. Mungu alitaka kujua kama kweli Abramu anampenda na ataacha vitu vyake vyote alivyokuwa navyo na aamini kwamba Mungu atamlinda.

3.2 Mungu alimwahidi Abramu vitu vya maana kadhaa ikiwa angemtii. Tunafanya ahadi kuonyesha kwamba tanamaanisha kufanya chenye tunasema. Tukifanya ahadi, ni vyema lazima kuona kwamba hatutavunja ahadi. Mungu akifanya ahadi, KILA MARA hutimiza hiyo ahadi.

Hii ni baadhi ya vitu vyenye Mungu aliahidi Abramu.

- Watoto wako na wajukuu wako hatimae watakuwa taifa kubwa.
- Nitakubariki na nifanye jina lako liwe na sifa.
- Siku moja watu wote wa ulimwengu watafurahi kwa sababu ya mmoja wa uzao wako.

Abramu aliamini kwamba Mungu atatimiza ahadi zake. Alijua kwamba yote aliyoahidiwa na Mungu yalikuwa ya dhamana kuliko marafiki na kila kitu kilichoko Uru.

3.3 Kwa hivyo Abramu alifanya vile Mungu alitaka. Alichukuwa mkewe Sarai na mpwa wake Lutu na kuondoka Uru wote. Ilikuwa vigumu kuacha nyuma marafiki wao, nyumbani kwao na mji wao walioupenda, lakini waliamini Mungu zaidi kwa hivyo walianza safari yao ndefu.

Safari ilikuwa ndefu, ngumu na hatari nyingi lakini Mungu alikuwa akiwalinda. Walipumzika kidogo kwa mji wa Harani na baadaye wakaendelea kusini kwa nchi ya Kanaani. (Nchi hii sasa inaitwa Israeli).

3.4 Abramu alipofika kwa nchi ya Kanaani, alijenga madhabahu na akatolea Mungu sadaka ya mwana kondoo kumshukuru kwa kumleta salama kwa nchi hii. Mungu alifurahi kwa sababu Abramu alimtii. Baadaye Mungu alimpa Abramu ahadi nyingine. Mungu aliahidi kwamba atampa Abramu pamoja na uzao wake nchi ya Kanaani milele.

3.5 Kwa hivyo, Mungu alitimiza hizi ahadi kwa Abramu? Ndiyo, alitimiza. Hebu tuzione na tuangalie vile zilikuwa za kweli.

- Wazao wa Abramu walikua na wakawa taifa la Wayahudi
- Mungu alibariki Abramu na jina lake likawa na sifa – bado tunajifunza juu yake hadi leo
- Yesu ni mmoja wa uzao wa Abramu. Yesu atakapokuja kusimamisha Ufalme wa Mungu, kila mtu atafurahi.

Lakini, na ahadi kwamba Mungu atampa Abramu na uzao wake nchi waishi milele? Abramu amekufa, kwa hivyo Mungu ametimiza ahadi yake kweli? Kweli, hii ndiyo ahadi ya maana sana kwa kila mtu – wakati Yesu atarudi hapa duniani atafufua Abramu kutoka kwa wafu. Halafu Abramu ataishi nchini milele kwa Ufalme wa Mungu.

Abramu aliacha nyumba na marafiki ili afurahishe Mungu. Lakini Mungu alimwahidi mambo ya ajabu mbadala – kuishi milele kwa Ufalme wa Mungu wa ajabu. Mungu ametuahidi hata sisi hizo ahadi. Tukimpenda na tujaribu kumtii, Mungu atatuwezesha kuishi kwa Ufalme Wake wakati Yesu atakapokuja. Kwa hivyo tujaribu sana kumpenda Mungu.